**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI) 1982**
***(NA 9 YA 1982)***
***(Zimetungwa chini ya kifungu cha 80 na 81)***

**SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA ZA (ADA YA VIBALI VYA UTAMADUNI NA BURUDANI) ZA MWAKA 2023**

| | | |
|---|---|---|
| ***Jina la sheria na tarehe ya kuanza kutumika*** | 1. | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba za (Ada za Vibali vya Utamaduni na Burudani) za mwaka 2023 na zitaanza kutumika mara zitakapotangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| ***Eneo zitakapotumika*** | 2 | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililoko chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.. |
| ***Tafsiri za maneno*** | 3 | Katika Sheria Ndogo hizi:<br>**“ada ya burudani”** maana yake ni kiasi cha fedha ambacho kinatozwa na Halmashauri kwa ajili ya kibali cha burudani, shughuli yoyote ya sherehe au michezo itakayofanyika katika eneo la Halmashauri;<br><br>**“Afisa Mtendaji”** maana yake ni Afisa Mtendaji wa Kata yoyote iliyomo katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.<br><br>**“Afisa Utamadumi”** maana yake ni Afisa Utumaduni wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba au Afisa yeyote aliyechaguliwa kutekeleza majukumu ya kiutamaduni.<br><br>**“Burudani”** shughuli au tukio lolote la kujumuisha watu likiwa na nia ya kuburudisha au kutoa ujumbe fulani.<br><br>**“Halmashauri”** maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.<br><br>**“Mkurugenzi”** maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashuri ya Wilaya ya Tandahimba au Afisa yeyote wa Halmashauri ya Wilaya anayekaimu nafasi ya Ukurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kwa wakati huo. |
| ***Utoaji wa*** | 4 (1) | Halmashauri ya wilaya itatoa vibali vya Burudani yoyote ambayo |

***vibali vya Burdani.*** itafanyika katika eneo lililomo katika himaya ya Halmashauri ya wilaya kama inavyoonyesha kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kila mtu anawajibu wa kuomba kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kabla ya kuendesha burudani ya aina yoyote.

(3) Kibali ambacho kitatolewa na Mkurugenzi wa Halmashuri kitaonyesha burudani itafanyika wapi, lini na muda wa kuanza na muda wa kumaliza.

***Wajibu wa kuomba kibali***

5 Kila mwananchi au taasisi atawajibika kuomba kibali cha burudani kabla hajaanza shughuli hiyo.

***Ada ya kiingilio katika michezo.***

6 Mapato yoyote yatokanayo na kiingilio cha katika michezo mbalimbali katika ngazi ya Taifa, Mkoa au Wilaya asilimia (5%) ya Mapato hayo yatakuwa ni ya Halmashauri ya Wilaya.

***Afisa wa Halmashauri kuingia na kukagua kibali***

7 (1) Afisa ambaye ametajwa katika Sheria Ndogo hizi ataweza kupita, kuingia katika sehemu yoyote ya burudani ambayo imetajwa katika Sheria ndogo hizi na kukagua kibali cha burudani.

(2) Endapo mwendeshaji wa Burudani hiyo atakuwa hana kibali, Afisa huyo ataweza kumtoza faini mtu huyo hapo hapo kwa kuendesha burudani bila kibali.\

(3) Endapo mwendeshaji wa burudani huyo atakataa au kushindwa kulipia ada hiyo ya burudani kama atakavyoelekezwa na Afisa wa Halmashauri, Afisa huyo wa Halmashauri anaweza kusimamisha na kufunga shughuli au burudani hiyo.

***Makosa na Adhabu***

8 Mtu yeyote au mwendeshaji wa burudani ambaye atakiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa la jinai na atashtakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili (200,000/=) na isiyozidi Milioni Moja (1,000,000/=) au kufungwa jela miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

***Mkuregenzi***

9 Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na uwezo wa kumtoza faini

| | | |
|---|---|---|
| ***kutoza Faini*** | | mtu yeyote atakayekiuka kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi, ambayo kimsingi haitazidi kiwango cha faini iliyomo katika kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi. |
| ***Halmashauri kufungua shauri la madai*** | 10 | Bila kuathiri yale yote yaliyoelezwa katika kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaweza kumfungulia mashataka ya madai mtu yeyote, Taasisi, Kampuni, Klabu au Shirika lolote lililoshindwa kuomba kibali kwaajili ya kufanya burudani au masuaa ya utamaduni. |
| ***Mkurugenzi kutoa mwongozo inapolazimu*** | 11 | Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na uwezo wa kutoa Mwongozo maalum ili kuweka mazingira yanayofaa kuboresha utekelezaji wa sheria Ndogo hizi wakati wowote ulazima utakapojitokeza. |
| ***Maombi ya vibali yawasilishwe kwa maandishi*** | 12 | Maombi yote kwa ajili ya vibali vya utamaduni na burudani chini ya sheria ndogo hizi, yatawasilishwa katika ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri, kwa maandishi. |
| ***Wajibu wa vikundi vya sanaa na muziki kujiajiri*** | 13 | Vikundi vyote vinavyoendesha shughuli za sanaa na muziki ndani ya Halmashauri vitawajibika kusajiliwa kwenye Halmashauri na kupewa hati ya usajili. |
| ***Vibali vitatumika na kikundi kimoja tu.*** | 14 | Vibali vya burudani vitakavyotolewa havitapaswa kuazimishwa kwa mtu au vikundi vingine ila yule au kikundi kile tu kilichokusudiwa. |
| ***Wajibu wa kuonyesha kibali kwa Afisa wa Halmashauri*** | 15 | Kila mwenye kibali atawajibika kuonyesha kibali chake wakati wowote atakapotakiwa kufanya hivyo na Afisa wa Halmashauri aliyeruhusiwa. |

## JEDWALI

Orodha ya aina za burudani zinazopaswa kuombewa vibali.

| Na | Aina ya burudani | Kiasi cha TSHs. |
|---|---|---|
| 1 | Promotion (matangazo ya kukuza biashara) | 30,000/= |
| 2 | Onyesho la Urembo (Miss) | 70,000/= |
| 3 | Onyesho la muziki | 30,000/= |
| 4 | Onyesho la michezo ya kuigiza | 30,000/= |
| 5 | Muziki wa dansi (Band) | 30,000/= |
| 6 | Muziki wa Disko | 30,000/= |
| 7 | Muziki wa Taarabu | 30,000/= |
| 8 | Sherehe ya Harusi au send off | 30,000/= |
| 9 | Sherehe ya kuagana na kukaribishana | 30,000/= |
| 10 | Sherehe ya kuaga na kukaribisha mwaka | 30,000/= kwa siku |
| 11 | Sherehe za mashirika na Taasisi mbalimbali | 30,000/= kwa tukio |
| 12 | Onyesho la video ya wazi | 20,000/= kwa siku |
| 13 | Matangazo ya mitaani kwa kutumia vipaza sauti | 20,000/= kwa siku |
| 14 | Sherehe ya ngoma ya harusi, mpeano au ngoma aina yoyote | 20,000/= kwa siku |
| 15 | Sherehe ya Mchiriku | 20,000/= kwa siku |
| 16 | Sherehe za jando na unyago | 20,000/= kwa siku |
| 17 | Mazinga ombwe. | 20,000/= kwa siku |
| 18 | Maonyesho ya sinema, video na mpira | 20,000/= kwa mwezi |
| 19 | Muziki wa asili | 30,000/= kwa siku |
| 20 | Wapiga picha za mnato na picha za video | 30,000/= kwa siku |
| 21 | Shindano la Mpira | 30,000/= mechi za nje<br>30,000/= mechi za ndani |
| 22 | Maonyesho ya Mavazi | 50,000/= |

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa azimio lililopitishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba katika kikao kilichoketi na kufanyika tarehe……………………… na ilibandikwa mbele ya:

…………………………………

**MARIAM SAID MWANZALIMA**

*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba*

…………………………………

**BAISA ABDALLAH BAISA**

*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba*

**NAKUBALI**

**…………………………………………………**

**ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB)**
**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS**
**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITA)**

**Dodoma,**
**Juni, 2023**